BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehma, kwa kutujaalia uzima na afya njema ambavyo vimetuwezesha kukutana tena katika Baraza hili la Kumi kwa lengo la kujadili na kuidhinisha Mapato na Matumizi ya Fedha za Serikali yetu. Aidha, nachukua fursa hii kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Baraza kwa kuliongoza Baraza hili kwa umahiri mkubwa na ninaamini kwamba mtaendelea kuliongoza Baraza hili kwa hekima, busara na uadilifu wa hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuiongoza nchi yetu kwa uadilifu, hekima na busara ambapo kumepelekea kupatikana kwa maendeleo pamoja na kuendelea kudumu kwa amani na utulivu katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** pia, sina budi kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Mheshimiwa Mwalimu Haroun Ali Suleiman kwa umahiri wake uliomfanya aweze kuteuliwa tena kuiongoza Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, nachukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yetu kwa umoja wao na kazi nzuri waliyoifanya kiasi cha kunirahisisishia kazi yangu ya kuongoza kikao kuwa nyepesi zaidi, kwa hakika ni Wajumbe mahiri, wameweza kuijadili ipasavyo na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha wanazoidhinisha kwa Wizara hii zinatumiwa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima ya hali ya juu kabisa napenda kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Hassan Khamis Hafidh | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Machano Othman Said | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Haji Jecha Salum | Katibu |
| 9. | Ndg. Salma Muhsin Haji | Katibu |
| 10. | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora katika kusimamia na kutekeleza Bajeti yake, inatekeleza jumla ya Mafungu *kumi (10)* ambayo ni:

*(i)* Fungu G 01 – Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora;
*(ii)* Fungu G 02 – Mahakama Kuu Zanzibar;
*(iii)* Fungu G 03 – Afisi ya Mwanasheria Mkuu;
*(iv)* Fungu G 04 – Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka;
*(v)* Fungu G 05 – Tume ya Kurekebisha Sheria;
*(vi)* Fungu *E 05* – Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi;
*(vii)* Fungu *E 07* – Kamisheni ya Utumishi wa Umma;
*(viii)* Fungu *E 04* – Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali;
*(ix)* Fungu *E 08* – Tume ya Utumishi Serikalini;
*(x)* Fungu A 02 – Ofisi ya Baraza la Mapinduzi.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, Kamati yetu haikujadili fungu la Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa vile fungu hilo lilipitiwa na Kamati ya PAC.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa Mkandarasi wa Jengo la Mahakama Kuu, Tunguu halipwi kwa wakati na kwa mujibu wa mkataba. Hivyo, Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuhakikisha kuwa inamaliza ujenzi wa Jengo la Mahakama Kuu huko Tunguu ambalo limechukuwa muda mrefu kukamilika kwake ili kuweza kutimiza lengo lililokusudiwa huku ikitiliwa maanani kwamba Jengo la Mahakama Kuu, Vuga

linazidi kuchakaa na halifai kutumiwa na Kiongozi wa Kitaifa kama Jaji Mkuu wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imegundua kuwa majengo mengi ya Mahakama ni machakavu na mabovu hayafai tena kutumika kwa shughuli za kimahakama kwa kukosa hadhi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuandaa mradi maalum utakaoshughulikia kuyafanyia matengenezo majengo ya Mahakama au kujenga mapya Unguja na Pemba kutokana na kuchakaa kwa majengo mengi na kuondoa ufinyu wa nafasi katika majengo yaliopo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika ziara zake mbali mbali kuangalia shughuli zinazofanywa na Wizara hii Kisiwani – Pemba, haikuridhishwa na utaratibu unaotumiwa na baaadhi ya taasisi zisizokuwa na Mafungu kupewa fedha za matumizi ya kawaida kwa njia ya mitandao ya kijamii kama vile tigo pesa na EzyPesa au kutoka afisa wa taasisi hiyo Unguja kwenda Pemba kwa ajili hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Wizara hii uwekwe utaratibu mzuri wa kuwaingizia fedha za matumizi mengineyo kwa usahihi taasisi zisizokuwa na mafungu za Pemba ili kuongeza ufanisi wa kazi kwa maendeleo endelevu ya Taifa hili.

**Mheshimiwa Spika,** Pia, Kamati imegundua kwamba Mahakama haina uhakika wala ushahidi wa deni wanalodaiwa na mashahidi wanaofika Mahakamani kutoa ushahidi katika kesi mbali mbali. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuingiza kwa wakati fedha kwa ajili ya kulipwa mashahidi ambao ni muhimu katika uendeshaji wa

kesi. Vile vile, Mahakama inashauriwa kuandaa mfumo wa uwekaji kumbukumbu za mashahidi wote pamoja na stahiki zao hasa katika Mahakama za Pemba ambapo idadi ya mashahidi haifahamiki na yumkini hata kiwango cha fedha wanachotakiwa kulipwa hakifahamiki.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia, imegundua Mahakama hawana vitendea kazi stahiki na viliopo vipo katika hali mbaya kutokana na uchakavu wake hali ambayo si nzuri hata kidogo kwa muhimili kama wa Mahakama kuendelea kufanya kazi katika mazingira yasiyoridhisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaiomba Serikali kuiona kadhia hii kwa jicho la karibu na uharaka ili muhimili wa Mahakama uendelee kutekeleza jukumu lake la kutoa haki za kisheria katika yetu ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu haikurishwa na mwenendo wa kesi za watuhumiwa wa Dawa Za kulevya Kisiwani Pemba, kwa kipindi cha mwaka mmoja jumla ya kesi 91 zimefikishwa katika Mahkama za Pemba, Hata hivyo ni Watuhumiwa wawili (2) tu ndio wamehukumiwa kifungo tena cha chini ya miezi tisa (9), hali ambayo imeleta mashaka kwa kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Mahkama zote za Zanzibar zitekeleze wajibu wake wa kutoa haki kulingana na sheria na taratibu zinavyoelekeza bila ya ubaguzi wowote. Pia, tunaomba vyombo husika vifatilie kwa ukaribu sana kuhusu kesi za madawa ya kulevya, Pemba.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuna kadhia ya Waislamu wanaotaka kutekeleza Ibada ya Hija kwa mwaka huu kutokana na kutokuwa na taarifa za uhakika kuhusu uwepo wa safari ya Hija.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaiomba Serikali kutoa tamko la hatma ya Waumini wa Dini ya Kiislamu waliojiandaa kwenda kuhiji Makka kama safari ipo au haipo ili waweze kujua na kujipanga mapema.

***HITIMISHO***

**Mheshimiwa Spika,** mwisho, napenda kuchukuwa fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu, kwa niaba ya Kamati pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa wakati wote wa uwasilishaji wa maoni yetu.

Kamati pia, inatoa shukrani zake za dhati kwa Katibu wa Baraza la Wawakilishi ndugu Raya Issa Msellem, Mratibu wa Shughuli za Kamati ndugu, Khamis Hamad Haji pamoja na watendaji wote kwa ujumla wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi ambao wameisaidia sana Kamati hii kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** nachukuwa nafasi hii ya pekee kuwashukuru kwa dhati kabisa Makatibu wetu wa Kamati ndugu Haji Jecha Salim na ndugu Salma Muhsin Haji kwa namna walivyoweza kutekeleza vyema majukumu yao katika kipindi chote cha uhai wa Kamati hii na wakati wa kujadili makadirio ya Bajeti hii.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia Kamati imeona kwamba majukumu mengi ya taasisi za Serikali hayawezi kufanyika ipasavyo kutokana na kutoingiziwa fedha kwa wakati na kwa mujibu wa kilichopangwa katika bajeti zao. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuingiza fedha kwa wakati na kama zilivyopangwa ili ufanisi wa kiutendaji uweze kupatikana kwa maendeleo ya wananchi na nchi yetu kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamechoka kwenda kwenye idara au taasisi za Serikali na kusikiliza changamoto juu ya changamoto, ni matumaini yetu hoja zetu hizi tulizoziona na kuziibua zitafanyiwa kazi kwa lengo la kuiletea maendeleo nchi yetu na wananchi wetu kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia kamati imeona kwamba majukumu mengi ya taasisi za Serikali hayawezi kufanyika ipasavyo kutokana na kutoingiziwa fedha kwa wakati na kwa mujibu wa kilichopangwa katika bajeti zao. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuingiza fedha kwa wakati na kama zilivyopangwa ili ufanisi wa kiutendaji uweze kupatikana kwa maendeleo ya wananchi na nchi yetu kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa, Kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako waichangie vyema Bajeti hii na hatimae waiidhinishie Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, makadirio ya fedha zilizopangwa kutumiwa katika mwaka wa fedha *2021/2022* ili wapate kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati yangu ***Naomba Kuunga Mkono Hoja.***

Ahsante,

……………………………….

**(Hassan Khamis Hafidh)**

Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

Baraza la Wawakilishi, **Zanzibar**